

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**  
**Hongera kwa Wafungwa Walioachiwa huru na Familia zao**  
**(Imetafsiriwa)**

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Ardhi Iliyobarikiwa ya Palestina inatoa pungezi na baraka zake kwa wafungwa walioachiliwa huru na familia zao baada ya kuachiliwa kutoka magereza ya madhalimu.

Huku tukimuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu awapunguzie dhiki wafungwa waliosalia, pia tunamuomba awapunguzie mateso wanaodhulumiwa na awatoe mahabusu kutoka katika jela za Mamlaka ya Palestina, chombo na tawi la usalama la Mayahudi. Tunamuomba Yeye awakomboe waliofungwa katika jela za madhalimu katika tawala dhalimu zinazotawala ardhi za Waislamu.

Pia tunamuomba Mwenyezi Mungu auruzuku Msikiti wa Al-Aqsa wanajeshi kutoka katika Umma wa Uislamu ambao watapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu na kuutakasa kutokana na Mayahudi, kama vile wanajeshi wa Salahuddin walivoutakasa kutokana na Makruseda. Tunaomba Ardhi Iliyobarikiwa iregee kwenye mamlaka ya Waislamu, ikiwa salama salimini kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu aliunganishe neno la Umma wa Muhammad (swt) chini ya utawala wa Kitabu Chake na bendera ya Mtume Wake (saw), katika kivuli cha Khilafah Rashida kwa njia ya Utume. Yeye ndiye Mlinzi wa hilo na Muweza wa kulitimiza.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir  
katika Ardhi Iliyobarikiwa – Palestina**